# NORTH EAST TANZANIA CONFERENCE

## OF SEVENTH DAY ADVENTIST CHURCH

## HUDUMA ZA FAMILIA NA WACHUNGAJI

# LISHA KONDOO WA MUNGU

# WACHUNGAJI, WAZEE NA MASHEMASI

**Imeandaliwa na Pr J.Lusega**

**MKURUGENZI HUDUMA ZA FAMILIA NA WACHUNGAJI**

**LISHA WANA-KONDOO WANGU**

**Namna Viongozi Wanavyoweza Kulitunza Kanisa**

***15****Walipokwisha kula, Yesu akamwuliza Simoni Petro, "Je, Simoni mwana wa Yohana, unanipenda kweli kuliko hawa?'' Yeye akamjibu, "Ndiyo, Bwana Wewe unajua ya kuwa ninakupenda.'' Yesu akamwambia, "Lisha wana-kondoo Wangu.''*
***16****Yesu akamwambia tena, "Simoni, mwana wa Yohana, wanipenda?'' Petro akamjibu, "Ndiyo Bwana, Wewe unajua ya kuwa ninakupenda.'' Yesu akamwambia, "Chunga kondoo Zangu.''*
***17****Kwa mara ya tatu Yesu akamwuliza Petro, "Simoni mwana wa Yohana, unanipenda?'' Petro akahuzunika sana kwa kuwa Yesu alimwuliza mara ya tatu, 'Unanipenda?' Akamjibu, "Bwana, Wewe unajua yote, unajua ya kuwa ninakupenda.'' Yesu akamwambia, "Lisha kondoo Zangu. (Yohana 21:15-17)*

*"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli." 2 Timotheo 2:15*

Agizo ambalo Petro alipewa na Kristo kabla ya kupaa kwake mbinguni lilikuwa "Lisha wanakondoo wangu" agizo hili amepewa kila kiongozi kanisani mchungaji mzee, shemasi na kadhalika.

Katika mafungu hayo hapo juu tunaweza kupata vidokezo muhimu vinavyohitajika kwa kila kiongozi wa Kanisa ili aweze kuwa mlishaji mzuri wa kundi lake **anapaswa kuwa watu wenye bidii katika mambo yote**, bidii katika,Kulisha **kondoo wa Bwana mkate toka mbinguni** mtembelee kondoo kwa haraka **hasa anapolia** akihitaji msaada wako.Tafuta kondoo **waliopotea ambao hawaji kundini.** Wajali, wapende wote na kuwathamini maana Bwana aliwafia na kuwapenda upeo.

**. Kiongozi afaaye kulisha wanakondoo wa Bwana**

1. Kwanza anapaswa awe mtu wa maombi na maandiko. Mtu wa maombi na maandiko ni yule aliye na ratiba yake pekee (personal devotion) na ya familia kusoma neno na kujifunza. Swali, tunasomaje na kujifunza?
    - Kusoma neno na kujifunza Biblia ianasema neno la Bwana ni hai tena lina nguvu (Ebrani 4:12) lina nguvu ya kubadili maisha (Yoh 6:63) tunapofungua biblia tunasikia sauti ya Mungu.Tunapokuwa na Biblia mkononi,ni sawa na kusimama mbele za Mungu maneno tunsyosoma ni sauti ya Mungu
    - Hivyo tunapaswa kusoma na kujifunza neno la Mungu kwa roho ya unyenyekevu ya mtu mwenye shauku ya kujifunza**."we must come with a humble and teachable spirit to obtain knowledge from the great I AM" (The Great Controversy, p 599**
    - Tunaposoma neno la Mungu tusifikirie mambo yetu ya kawaida kuepuka hilo tuchague muda ufaao kwa maombi ya pekee na ya familia, muda usio na shughuli wakati mawazo yanapokuwa na utulivu, uwezo na nguvu *"Tulieni, mjue*

*ya kwamba mimi ndimi Mungu, nitatukuzwa katikati ya mataifa, nitatukuzwa katika dunia.''* (Zaburi 46:10)

- Kusoma na kujifunza Biblia kwa kawaida huanza na maombi tunapaswa kumwalika Roho yuleyule aliyewavuvia wandishi wa Biblia kutuvuvia na sisi katika akili zetu ili kuelewa na kufanya mapenzi ya Mungu
- Kama una kamusi itumie kujua tafasiri maneno au sentensi ngumu. Tumia biblia mbalimbali kupanua maana ya aya unazosoma kasha thibitisha na roho ya unabii kabla hujapanda mimbarani kuhubiri
- Unapokutana na mambo yanayoelezwa kinyume na mazoea yako usiruke na kutafuta sehemu nyingine tunyenyekee na kukusanya maujumbe yote yaani tumwache Mungu atutengeneze
- Unaposoma na kujifunza pata muda wa kutafakari na kuomba roho afunue mapenzi ya Mungu na wala usilazimishe maandiko kusema unachotaka wewe bali tuache neno liongee kwa uwazi na kuleta maana yake kamili.
- Unaposoma na kujifunza uwe na daftari (Note Book) kuandika vitu vipya na muhimu kwa ajili ya maisha yako na kwa ajili ya kufundisha familia yako na kundi la kondoo wa Bwana uliokabidhiwa kanisani
- Baada ya kujilisha vizuri na kujisikia una kitu sasa unaweza kutokea mbele za kondoo wa Bwana ukawalisha kitu cha maana. Kama nilivyotangulia kusema kusoma kusoma na kujifunza hutanguliwa na maombi hii hufanya mtiririko wa maongozi ya Roho kwa watu wake wenye maneno matatu ya kingereza yaani **1.Revelation 2. Inspiration. 3. Ilumination – elezea**

Roho ya unabii inakazia hayo kwa kusema:
Soma biblia kwa bidii hasa kitabu cha Daniel na ufunuo ili kujua dalili na nyakati uweze kutahadharisha kundi lako mapema kabla hatari. Jitahidi kuwa mtu wa maombi

"Wachungaji ambao wangeweza kufanya kazi ya kufanikiwa kwa ajili ya wokovu war oho za watu hawana budi kuwa wanafunzi wa biblia na watu wenye kumwomba Mungu. Ni dhambi kuacha kusoma neon la Mungu huku tukijaribu kulifundisha kwa wengine…" (Wajumbe wa Kristo Uk 28)

"Yawapasa wahubiri kulitoa neon lile lililo imara la unabii kama imani ya msingi ya waadventista wa sabato, unabii wa Danieli na ufunuo wapasa kusomwa sana kwa ungalifu pamoja na maneno yasemayo "Tazama mwana kondoo aichukuaye dhambi ya ulimwengu" (Wajumbe wa Kristo Uk 50)." (Angalia pia Matukio ya Siku za Mwisho Uk 14 – 15)

2. Lishe ya Wana Wanakondoo wa Bwana

Wahubiri wengi leo wanahubiri wanavyoviona, wanavyosikia na vitu wanavyofurahia wasikilizaji wao. Lakini wanaiacha mioyo yao ikiwa na njaa. Wengine nao wanahubiri hadithi na vichekesho tu na sio neno la Mungu.

" Wanawaambia waonaji, "Msione maono tena!'' Nako kwa manabii wanasema, ''Msiendelee kutupatia maono ambayo ni ya kweli! Tuambieni mambo ya kupendeza, tabirini mambo ya uongo." (Isaya 30:10) – Wahubiri wa aina hii ndio wapendwao leo

Kondoo wa Mungu wanapaswa kula chakula cha kiroho, hawawezi kuwa hai bila chakula hicho,Yesu alisisitiza juu ya hilo. Mara tatu alimwagiza Petro kulisha kondoo wake na wanakondoo. Kamwe Petro hakusahau agizo hili kubwa alipoandika barua yake kwa makanisa Ili kundi lipate kushiba na kuwa na afya njema lazima lilishwe kikamilifu. Na chakula kikuu cha namna hiyo ni lazima kiandaliwe na kiongozi wa kundi wachungaji wazee wa Kanisa na mashemasi.alisema

"lichungeni kundi la Mungu mlilokabidhiwa, mkitumika kama waangalizi, si kwa kulazimishwa bali kwa hiari, kama Mungu anavyowataka mwe, si kwa tamaa ya fedha, bali mlio na bidii katika kutumika. Msijifanye mabwana juu ya wale walio chini ya uangalizi wenu, bali iweni vielelezo kwa hilo kundi" ( 1Petro 5:2 – 3).

Jilindeni nafsi zenu na mlilinde lile kundi lote
ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi wake. Lichungeni kanisa lake Mungu alilolinunua kwa damu yake mwenyewe.

3. Kiongozi Anatakiwa awe Kielelezo

Biblia inasema "Lazima aweze kuisimamia nyumba yake mwenyewe vizuri na kuhakikisha kwamba watoto wake wanamtii na kuwa na heshima kwa kila njia. 5(Kwa maana kama mtu hajui jinsi ya kusimamia nyumba yake mwenyewe atawezaje kuliangalia kanisa la Mungu?" (1Timotheo 3:4 - 5)

Pamoja na maandalizi yote yanayoweza kufanywa kwa ajili ya ulishaji wa kondoo bado kama kiongozi hawezi kuwa mfano kielelezo kwa kondoo zake hatatafanikiwa. Ili uweze kufanikiwa vizuri zingatia haya yafuatayo

a) Simamia familia yako vizuri kiroho na kuitiisha
b) Jali mikutano ya ibada usishughulike na mambo mengine wakati wa ibada – siku ya sabato
c) Wapende na kuwajali watu unaowaongoza
d) Wasaidie kwa mahitaji yao ya kiroho bila upendeleo
e) Wanaostahili kuonywa na kukaripiwa waonywe

**Wajibu wa Kanisa**

"Mungu huwawajibisha watu wake, kama jumuiya, kwa ajili ya dhambi zilizo ndani ya watu binafsi walio miongoni mwao. Viongozi wa kanisa wakipuuza kuchunguza kwa makini dhambi zinazoleta hasira ya Mungu dhidi ya jumuiya, watawajibika kwa ajili ya dhambi hizo."—3T 269.

"Kusingekuwa na marudi na utawala wa kanisa, kanisa lingepasuka vipande vipande; lisingeweza kushikamana kama jumuiya."—3T 428.